Watu Waliyojiandaa Kwa Ajili Ya Bwana

na

Ellis P. Forsman

Watu Waliyojiandaa Kwa Ajili Ya Bwana

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 8, 2011

Watu Waliyojiandaa Kwa Ajili Ya Bwana

Math. 3:1-17

Mungu alisema atamuinua nabii atakaye andaa njia ya Bwana.

Malaki 3:1, *"Angalieni namtuma mjumbe wangu, naye ataitengeneza njia mbele yangu, naye Bwana mnayemtafuta atalijilia hekalu lake ghafula; naam, Yule mjumbe wa agano mnayemfurahia angalieni, anakuja asema Bwana wa majeshi."*

Nabii huyo alikuwa Yohana mbatizaji.

Luka 1:76, *"Nawe motto utaitwa nabii wake aliye juu, kwa maana utatangulia mbele za uso wa Bwana, umtengenezee njia zake."*

Na, kupitia mahubiri yake hivyo ndivyo alivyofanya.

Math.3:1-3, *"Siku zile aliondokea Yohana Mbatizaji akihubiri katika nyika ya Uyahudi, na kusema, tubuni kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia. Kwa sababu huyo ndiye aliyenenwa na nabii Isaya, akisema, sauti ya mtu aliaye nyikani, itengenezeni njia ya Bwana, yanyosheni mapito yake."*

Kile ambacho kinajulikana kidogo ni kwamba Yohana pia alikuwa na kusudi ambalo lili kwenda bega kwa bega na ile ya kwanza:

Luka 1:17, *"Naye atatangulia mbele zake katika Roho ya Eliya na nguvu zake ili kuigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto, na kuwatilia waasi akili za wenye haki, na kumwekea Bwana tayari watu waliotengenezwa."*

Tutaona kile ambacho Yohana alifanya kilicho andaa watu wa Mungu kwa Bwana. Pia tutaona jinsi tunavyo paswa kuwa watu waliojiandaa kwa ajili ya Bwana.

Kazi ya Yohana Mbatizaji

Kwanza: Yohana Mbatizaji angekuwa "mkuu katika uso wa Bwana."

Luka 1:15, *"Kwa sababu atakuwa mkuu mbele za Bwana; hatakunywa divai wala kileo, naye atajazwa Roho Mtakatifu hata tangu tumboni mwa mamaye."*

Mwanadamu anaona mafanikio makubwa kupitia "macho ya ulimwengu": uchumi – wa kijamii.

Mungu, hata hivyo, anaona ukuu kutoka katika mtazamo wa kiroho.

- Luka 7:24-28, *"Basi wajumbe wa Yohana walipokwisha ondoka, alianza kuwaambia makutano habari za Yohana, mlitoka kwenda nyikani kutazama nini? Unyasi ukitikiswa na upepo? Lakini mlitokea kwenda kuona nini? Mtu aliyevikwa mavazi mororo? Jueni, watu wenye mavazi ya utukufu, wanao kula raha wamo katika majumba ya kifalme. Lakini mlitoka kwenda kuona nini? Nabii? Naam, nawambia, na aliye zaidi ya nabii huyo ndiye aliyeandikiwa haya. Tazama namtuma mjumbe wangu mbele ya uso wako, atakayeitengeneza njia yako mbele yako. Name nawaambia, katika wale waliozaliwa na wanawake hakuna aliye mkuu kuliko Yohana, lakini aliye mdogo katika ufalme wa Mungu ni mkuu kuliko yeye."*

- 1 Samweli 16:7, *"Lakini Bwana akamwambia Samweli, usimtazame uso wake, wala urefu wa kimo chake; kwa maana mimi nimemkataa. BWANA haangalii kama binadamu aangaliavyo; maana wanadamu huitazama sura ya nje, bali BWANA huu tazama moyo."*

Ukuu wa Yohana ulikuwa kwa sababu angeweza kujitenga kabisa na akajitoa kwa Bwana, toka tumboni mwa mamaye.

- Luka 1:15, *"Kwa sababu atakuwa mkuu mbele za Bwana; hatakunywa divai wala kileo; naye atajazwa Roho Mtakatifu hata tangu tumboni mwa mamaye.*

- Luka 1:5-6, *"Zamani za Herode, mfalme wa Uyahudi, palikuwa na kuhani mmoja , jina lake Zakaria, wa zamu ya Abiya na mkewe alikuwa mmoja wapo wa uzao wa Haruni jina lake Elisabeti. Na wote wawili walikuwa wenye haki mbele za Mungu,wakiendelea katika amri zote za Bwana na maagizo yake bila lawama."*

- Luka 1:41, *"Ikawa Elizabeti aliposikia kule kuamkia kwake Mariamu, kitoto kichanga kikaruka ndani ya tumbo lake; Elizabeti akajazwa Roho Mtakatifu."*

- Luka 1:67, *"Na baba yake Zakaria alijazwa na Roho Mtakatifu, na akafanya unabii,...."*

Kazi ya Yohana iliandikwa katika:

Luka 1:16-17, *"Na wengi katika Waisraeli atawarejeza kwa Bwana Mungu wao. Naye atatangulia mbele zake katika roho ya Eliya, na nguvu zake, ili kuigeuza mioyo ya baba, iwaelekee watoto, na kuwatilia waasi akili za wenye haki na kumwekea Bwana tayari watu waliotengenezwa."*

Kama siku za Eliya, wengi wa Waisraeli walikuwa hawaishi kwa ajili ya Bwana, bali kulingana na tumbo zao.

- Malaki 4:5-6, *"Ikumbukeni Torati ya Musa, mtumishi wangu, niliyomwamuru huko Horebu kwa ajili ya Israeli wote, naam, amri na hukumu. Angalieni nitawapelekea Eliya nabii, kabla haijaja siku ile ya BWANA iliyo kuu na kuogofya. Naye ataigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto wao, na mioyo ya watoto iwaelekee baba zao, ili nisije nikaipiga dunia kwa laana."*

- Math. 11:10-14, *"Huyo ndiye aliyeandikiwa haya, tazama mimi namtuma mjumbe wangu, mbele ya uso wako, atakayeitengeneza njia yako mbele yako. Amin,nawaambieni, hajaondokea mtu katika wazao wa wanawake aliye mkuu kuliko Yohana Mbatizaji, walakini aliye mdogo katika ufalme wa mbinguni ni mkuu kuliko yeye. Tangu siku za Yohana Mbatizaji hata sasa ufalme wa mbinguni hupatikana kwa nguvu, nao wenye nguvu wauteka. Kwa maana manabii wote na torati walitabiri mpaka wakati wa Yohana. Na ikiwa mnataka, yeye ndiye Eliya atakayekuja."*

Angerudisha unyenyekevu kwa Israeli kwa kugeuza mioyo ya baba ziwageukie watoto wao.

Ukamilifu wa kazi ya Yohana — ukizingatia watu wa Mungu — ili kuwa ni kuwaandaa kwa ajili ya Bwana.

Watu waliitaji kutubu na kugeuza mioyo yao kwa Mungu.

Math. 3:1-3, "*Siku zile aliondokea Yohana Mbazaji akihubiri katika nyika ya Uyahudi, na kusema, tubuni kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia. Kwa sababu huyo ndiye aliyenenwa na nabii Isaya, akisema, sauti ya mtu aliaye nyikani, itengenezeni njia ya Bwana, Yanyosheni mapito yake."*

Watu waliitaji kuangalia vitu jinsi Mungu alivyoziangalia: kiroho.

Math.3:7-12, *"Hata alipoona wengi miongoni mwa Mafarisayo na Masadukayo wakiujia itakayokuja? Basi zaeni matunda yapasayo toba; wala msiwaze mioyoni mwenu kwenda kwamba, tunaye baba, ndiye Ibrahimu; kwa maana nawambia ya kwamba Mungu aweza katika mawe haya kumuinulia Ibrahimu watoto. Na shoka lime kwisha kuwekwa penye mashina ya mti; basi kila mti usiozaa matunda mazuri hukatwa na kutupwa motoni. Kweli mimi nawabatiza kwa maji kwa ajili ya toba; bali yeye ajaye nyuma yangu ana nguvu kuliko mimi, wala sistahili hata kuvichukua viatu vyake; yeye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa moto. Ambaye pepeto lake li mkononi mwake, naye atausafisha uwanda*

wake; na kuikusanya ngano yake ghalani bali makapi atayateketeza kwa moto usiozimika."

Bwana alipokuja, aliwafundisha kutokana na muelekeo huu, na wale ambao kweli walimsikiliza Yohana walikuwa tayari kuamini na kufuata mafundisho ya Mwokozi wetu.

Kazi ya uinjisti leo

Kuna watu katika ulimwengu wa kidini wanaofundisha neno la Mungu "ni wakuu mbele ya macho ya Bwana." Watu wengiwanahitaji "mahubiri makuu" yanayo wa sisimua ili wajisikie vizuri.

1 Wakor. 2: 1-5, *"Basi ndugu zangu, mimi nilipokuja kwenu sikuja niwahubiri siri ya Mungu kwa ufasaha wa maneno, wala kwa hekima. Maana naliazimu nisijue nano lolote kwenu ila Yesu Kristo, naye amesulubiwa. Name nalikuwako kwenu katika hali ya udhaifu na hofu na matetemeko mengi. Na neno langu na kuhubiri kwangu hakukuwa kwa maneno ya hekima yenye kushawishi akili za watu, bali kwa dalili za Roho na nguvu, ili imani yenu isiwe katika hekima ya wanadamu, bali katika nguvu za Mungu."*

Wengi wanataka watu "wakubwa kati ya wanadamu" ili wawahubirie.

Math. 3:4, *"Naye Yohana mwenyewe alikuwa na vazi lake la singa za ngamia, na mshipi wa ngozi kiunoni mwake; na chakula chake kilikuwa nzige na asali ya mwitu."*

Kinacho wafanya waalimu wa Mungu kuwa wakuu ni kwamba wanajitenga wenyewe kumkaribia Bwana, badala ya kuwapendeza wanadamu.

Kusudi la kuhubiri ni kuwabadilisha watoto wa Mungu- ambao siyo waaminifu- kwa Bwana Mungu wetu.

- Kuna wale ambao hawampendi Bwana Mungu wetu kwa mioyo yao yote, nafsi na akili.
- Kuna wale wanaotembea kwa siri katika dhambi.
- Kuna wale walioko kimwili.
- Wapo wanaotembea kiunafiki.

Kufundisha kikamilifu au kuhubiri: inawaandaa watu wa Mungu kwa ajili ya Bwana: Karipia, kemea, na kuonya kwa uvumilivu wote.

2 Tim. 4:2, *"Lihubiri neno uwetayari wakati ukfaao na wakati usiokufaa, karipia, kemea, na kuonya kwa uvumilivu wote na mafundisho."*

Karipia watu wa Mungu kwa imani. Wale wanao penda Mungu atawageuza kutoka dhambini na kuwahimiza katika imani kwa Mungu: watakuwa wameandaliwa kwa ajili ya Bwana.

Hitimisho

Yohana kimsingi aliandaa njia ya Bwana, lakini kwa msimamo huo Mungu pia alimtaka Yohana aandae watu wake kwa ajili ya Bwana.

Umeshajiandaa?

Imani. Waeb. 11: 6, *"Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza, kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao."*

Tubu. Matend. 17:30, "*Basi zamani zile za ujinga Mungu alijifanya kama hazioni; bali sasa anawaagiza watu wote wa kila mahali watubu."*

Kiri. Waru. 10: 9-10, *"Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako yakuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu."*

Ubatizo.

- Marko 16:16, *"Aaminie na kubatizwa ataokoka, asiyeamini atahukumiwa."*
- Yoh. 3:5, *"Yesu akajibu Amin, amin, nakuambia, mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho; hawezi kuingia ufalme wa Mungu."*
- Matend.2:38, *"Petro akawambia, tubuni, mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, na mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."*
- Matend. 22:16, *"Unakawilia nini? Simama, ubatizwe na uoshwe dhambi, ukiliitia jina la Bwana."*